




Darasa la 1

Kitabu cha hadithi 3

Kiswahili

★ **Faida za Ng'ombe**

★ **Siku za Wiki**




Tusome Early Literacy Programme

Faida za Ng'ombe

Mwandishi: **Emolem Silas**

Mchoraji: **Simon Ndonge**



Huyu ni ng'ombe.

Ng'ombe ni mnyama wa nyumbani.

Ng'ombe ana faida nyingi.



Mama hukama ng'ombe wetu.

Ng'ombe hutupa maziwa.

Mimi ninapenda kunywa maziwa.





Ng'ombe hutupa nyama.

Nyama ya ng'ombe ni tamu.

Mimi hula nyama.

Ng'ombe hutupa ngozi.

Ngozi hutumiwa kutengeneza
sehemu ya juu ya ngoma.

Mimi ninapenda kupiga ngoma.





Ng'ombe hutupa mbolea.

Mbolea hutumika shambani.

Baba humwaga mbolea shambani.

Maswali

1. Taja vitu vinne tunavyopata kutokana na ng'ombe.
2. Ngozi ya ng'ombe hutumiwa kutengeneza nini?
3. Mbolea ya ng'ombe hutumika wapi?

Siku za Wiki

Mwandishi: **Stephen Kwoma**

Mchoraji: **Simon Ndonye**

Jumapili sisi huenda kanisani.

Sisi hufurahi sana siku ya Jumapili.





Jumatatu sisi huenda shuleni.

Tukiwa shuleni sisi husoma kwa bidii.



Jumanne sisi hucheza mpira shuleni.

Sisi hufurahia kucheza mpira.



Jumatano sisi huogelea shuleni.

Watoto hufurahia Jumatano sana.

Alhamisi sisi hucheza mchezo wa kuruka kamba.

Wasichana huufurahia sana mchezo huu.





Ijumaa sisi hupandisha bendera.

Sisi huimba wimbo wa taifa.



Jumamosi sisi hukaa nyumbani. Sisi hucheza michezo tofauti. Pia sisi huwasaidia wazazi kwa kazi za nyumbani.

Maswali

1. Taja siku saba za wiki.
2. Watoto hupandisha bendera shuleni siku gani?
3. Watoto hufanya nini siku ya Alhamisi?

Darasa la 1

Kitabu cha hadithi 3

★ Faida za Ng'ombe

★ Siku za Wiki

Vitabu vya hadithi vya **Tusome** vimeandikwa kwa ustadi wa hali ya juu ili kusaidia kuinua kiwango cha kusoma kwa wanafunzi wa darasa la 1 na la 2. Hadithi hizi zinawapa wanafunzi nafasi ya kufurahia hadithi na kuinua uelewa wa hadithi nje ya masomo ya kawaida darasani. Vitabu hivi vinaweza kutumiwa na yeyote anayejifunza Kiswahili. Tunashukuru kwa usaidizi wa SIL LEAD kwa mchango wao katika kuandika hadithi hizi. Ili kusaidia katika juhudi hii, hadithi hizi zimeandikwa kwa kuzingatia yafuatayo:-

- Lugha rahisi kwa wanafunzi na sentensi zenye urefu unaofaa,
- Picha za kuvutia ambazo hazielezi hadithi kikamilifu lakini zinamwezesha msomaji kusoma zaidi ili aelewe hadithi,
- Hadithi za kufurahisha zenye maudhui na dhamira ambazo msomaji anayeanza kusoma ataweza kulinganisha na maisha yake ya kila siku,
- Vichwa vya hadithi ambavyo vinamwezesha msomaji kutabiri.

Hadithi katika msururu huu ni:

- Darasa la 1:**
- ▶ Fisi Mjinga **na** Chura na Kiboko
 - ▶ Mchezaji Banda **na** Kisa cha Simba na Mbuni
 - ▶ Faida za Ng'ombe **na** Siku za Wiki
 - ▶ Kwa nini Mzee Kobe ana magamba **na** Jitu la Mtoni

- Darasa la 2:**
- ▶ Shujaa Musa **na** Mnyama Nimpendaye
 - ▶ Mama Mzee na Nguruwe **na** Juma na Sungura
 - ▶ Fisi na Mbuzi **na** Kuku na Mwewe Wakosana
 - ▶ Sababu ya Paka Kupenda Kukaa Jikoni **na** Kwa nini Twiga ana Shingo Ndefu
 - ▶ Safari ya Mombasa **na** Masaibu ya Musa



USAID
FROM THE AMERICAN PEOPLE



UKaid
from the British people

Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.